KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 18, Issue 2
19th Safar 1433
13th Jan, 2012

JILBAAB YA MWANAMKE WA KI-ISLAMU

Na Sheikh Muhammad Naasir ud Deen al-Albaani (رحمه الله)

MAKOSA YA KIMSINGI YA WENYE KUSEMA YAKWAMBA KUJIFUNIKA USO KWA MWANAMKE NI WAAJIB.

1. Tafsiri ya 'al-idnaa' katika Aya ya Jilbaab kumaanisha "kujifunika uso."

Tafsiri hii ya ki-makosa ni kinyume cha maana ya kimsingi ya neon la kiarabu, lenye maana ya "kuja karibu" kama ilivyotajwa kwenye kamusi zenye kutegemewa kama vile **al-Mufradaat** cha Mwanachuoni maarufu, ar-Raaghib al-Asbahaani. Hatahivyo, kuna dalili zenye kutosheleza kwenye tafsiri ya mfasiri anayeongoza wa Qur'an, Ibn 'Abbaas, aliyeifasiri Aya isemayo , "Na alilete Jilbaab karibu na uso wake pasi na kuufunika." Inatakiwa hapa itambulike yakwamba hapana riwaya yoyote iliyo swaheeh, iliyotumiwa kama dalili zenye kuikosoa tafsiri hii.

2. Tafsiri ya jilbaab kuwa ni "kitambara chenye kufunika uso."

Kama tafsiri iliyotangulia ya kimakosa, tafsiri hii haina msingi ki-Lugha. Ni kinyume cha tafsiri ya wanavyuoni wakubwa, wa zamani waliopita na wa sasa tulio nao, walioeleza jinsi ilivyo Jilbaab kuwa ni kitambara ambacho wanawake hujitanda juu ya vitambara vyao vya kichwa (khimaar). Hata Sheikh at-Tuwaijree mwenyewe ameinukuu tafsiri hii kutoka kwa Ibn Mas'ood na wanavyuoni wengine wa ki-Salafee. Al-Baghawee ameitaja kuwa ndiyo tafsiri ya kisawasawa katika tafsiri yake (vol. 3, uk. 518) akasema, "Ni nguo ambayo mwanamke hujifunika nayo, na huvaliwa juu ya nguo (dir ') na kitambara cha kichwa." Vilevile amesema Ibn Hazm, "Jilbaab katika lugha ya kiarabu ambayo Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyotuzungumzia sisi ni chenye kufunika mwili mzima na wala sio sehemu fulani tu." (vol. 3, uk. 217). Al-Qurtubee akaitangaza hii kuwa ndiyo ya sawa kwenye tafsiri yake na Ibn Katheer akasema, "Ni kile kitambara kinachovaliwa juu ya kitambara cha kichwa." (vol. 3, uk. 518)

3. Madai yakwamba Khimaar (kitambara cha kichwa) ndio yenye kufunika kichwa na uso.

Katika kufanya hivyo "uso" utakuwa umeongezwa kiholela kwenye maana yake ili Aya iwe na maana: "Na wanig'inize vitambara vyao vya kichwa juu ya vifua vyao" ionekane kuwapendelea kwenye tafsiri zao, haliyakuwa kwa hakika si hivyo. Neno "Khimaar" ki-lugha maana yake ni kitambara cha kichwa tu. Kila kinapotajwa kwa matamshi ya ujumla, hili ndilo linalokusudiwa. Kwa mfano katika hadeeth ya kupangusa (mas-h) juu ya khimaar na matamshi ya ki-Utume: "Swala ya mwanamke aliyepita umri wa kubaleghe haitokubaliwa bila ya khimaar." Hadeeth hii inathibitisha kubatilika kwa tafsiri zao za kimakosa, kwa sababu hata wale wenye kupituka mipaka wenyewe - licha ya wanavyuoni - huitumia kuwa ni dalili yakwamba mwanamke kujifunika uso kwenye swala ni sharuti katika kujuzu kwake. Wao wanaitumia kuwa ni dalili kwa kufunikia uso peke yake. La ziyada ni kwamba, tafsiri yao ya Aya ya Qawaa'id "… kuvua nguo zao" kumaanisha "jilbaab" inazidi kuyathibitisha hayo. Wao wanashikilia yakwamba inaruhusiwa kwa wanawake wakongwe kujitokeza mbele ya waume wenye kuruhusiwa kuowana nao, wakiwa na vitambara vya kichwa na nyuso zao zikiwa wazi. Mmojawapo miongoni mwa wanavyuoni wao wakubwa aliyatangaza hayo waziwazi. Amma kumuhusu Shaykh at-Tuwaijree, alidokeza hilo pasi na kulitamka kihakika. Baada ya kufanya utafiti wa kina juu ya rai za wanavyuoni wa zamani na wa sasa katika Nyanja zote za ki-ilimu, nimegundua yakwamba wao wote wameafikiana yakwamba khimaar ni kitambara cha kichwa. Nimeyataja majina ya zaidi ya wanavyuoni ishirini, miongoni mwao wakiwemo baadhi ya ma-Imaam wakubwa na wanavyuoni wa hadeeth. Kwa mfano, Abul-Waleed al-Baajee (f. 474 AH) aliyeongeza ziyada kwenye ufafanuzi wake, "Hairuhusiwi kuonekana kwake mbali na duara au mviringo wa uso wake."

4. Madai ya kongamano lililoafikiana (Ijmaa') yakwamba uso uzingatiwe kuwa ni 'awrah.

Shaykh at-Tuwaijree amedai kuwa wanavyuoni wameshikilia msimamo yakwamba uso wa mwanamke ulikuwa ni 'awrah na wengi ambao hawana ilimu, wakiwemo baadhi ya wenye Ph.D, wamemfuata yeye ki-Upofu. Kwa hakika, hayo ni madai ya urongo, ambao hapana yoyote aliyemtangulia kwenye madai hayo. Vitabu vya wanavyuoni wa ki-Hanbali ambao aliosoma kwao, pasi na kutaja vile vya wasiokuwa wao, vina dalili zenye kutosheleza juu ya urongo wake. Mimi nimezitaja nakala zao nyingi kwenye Ar-Radd. Kwa mfano, Ibn Hubayrah al-Hambalee amesema katika kitabu chake, al-Ifsaah, yakwamba uso hauzingatiwi kuwa ni 'awrah katika vyuo vitatu vikubwa na akaongezea, "Vilevile ni msimamo wa ki-riwaya wa Imam Ahmad." Wanavyuoni wengi wa ki-Hanbali wamechagua na kuifadhilisha riwaya hii katika vitabu vyao, kama vile Ibn Kudaamah katika al-Mughnee amefafanua sababu ya chaguo lake aliposema, "kwa sababu haja inalazimisha yakwamba uso usifunikwe kwa ajili ya kuuza na kununua, na mikono isifunikwe kwa ajili ya kutoa na kupokea." Miongoni mwa wanavyuoni wa ki-Hanbali, ni huyu mwanachuoni mkubwa, Ibn Muflih al-Hambalee ambaye Ibn al-Qayyim al-Jawziyyah aliyemsema, "Hapana yoyote aliye chini ya kuba la

YALIYOMO
JILBAAB YA MWANAMKE 1 - 4

Mbingu mwenye ilimu kuhusu Chuo cha Imaam Ahmad kuliko Ibn Muflih." Na mwalimu wake, Ibn Taymiyyah, alimwambia siku moja, "Wewe si Ibn Muflih, bali wewe ni Muflih!." Sina budi niwatajie matamshi ya Ibn Muflih ili wasomaji wapate kufaidika na ilimu pamoja na faida nyingi zilizomo ndani yake. Yaliyomo ndani yake ni ziyada ya kuyathibitisha yale madai ya urongo ya Sheikh at-Tuwaijree (jambo lenye kuashiriya yakwamba yeye alikuwa akiyafahamu hayo, lakini akaficha kwa kusudi ushahidi huu muhimu sana kwa wasomaji wake, haliyakuwa anadhihirisha madai yaliyo kinyume chake). "Jee ni sawa kuwaaibisha wanawake wenye kuweza kuolewa iwapo watadhihirisha nyuso zao kwenye mabarabara?" Jawabu itategemea iwapo ni waajib kwa wanawake kuziba nyuso zao au iwapo ni waajib kwa wanaume wainamishe macho yao badala ya kumwangalia. Kuna misimamo miwili katika suala hili. Kuhusiana na hadeeth ya Jareer ambamo alimosema: "Nimemuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu kutizama kwa ghafula bila ya kuwa muangalifu nae akaniamrisha mimi niangalie kando." Al-Qaadhi 'iyyaadh akasherehesha, "Wanavyuoni (رحمهم الله), wamesema yakwamba kuna ushahidi hapa kwenye hadeeth hii yakwamba si wajibu kwa mwanamke kujifunika uso wake njiani. Na badala yake, ni katika Sunnah iliyokokotezwa kwake kufanya hivyo na ni wajibu kwa mwanamume kuinamisha macho yake badala ya kumwangalia wakati wowote, isipokuwa kwa mas'ala yaliyoruhusiwa na sheriya. Sheikh Muhyud-deen an-Nawawee ameyataja hayo bila ya kuyasherehesha zaidi." Kisha al-Muflih akataja mazungumzo ya Ibn Taymiyyah ambayo aliyoyategemea at-Tuwaijree katika kitabu chake (Uk. 170), huku akijifanya hamnazo kuhusu maneno ya jamuhuri ya wanavyuoni. Maneno kama yale ya al-Qadhi 'iyyaadh na muafaka wa an-Nawawee katika kukubaliana nayo. Kisha al-Muflih akasema, "Juu ya msingi huo, jee yafaa kisheriya kumuadibu mtu (kumtia adabu)? Kumuadibu mtu hairuhusiwi kwenye mas'ala ambayo ndani yake kunapatikana ikhtilafu ya rai, na ikhtilafu ishatajwa kuwepo kwake. Na kuhusu rai yetu na rai ya kundi la wanavyuoni wa ki-Shaafi'ee na wengineo, kuwaangalia wanawake wanaofaa kuolewa bila ya matamaniwa au katika hali ya kujitenga (upweke) inaruhusiwa. Kwahiyo kumuadibu mtu si jambo la sawa."

Jawabu hili linakwenda sambamba na kauli ya Imaam Ahmad, "Hairuhusiwi kwa mwanachuoni kuwalazimisha watu wafuate rai (madh-hab) yake." Na hii ni iwapo haki iko upande wake. Jee huwaje ikiwa hali ni kwamba mwanachuoni huwapoteza watu kwa majivuno, udanganyifu na hata kuwatangaza Waislamu wengine kuwa ni makafiri kama alivyofanya at-Tuwaijree katika ukurasa wa 249 wa kitabu chake aliposema, "Yoyote mwenye kuwaruhusu wanawake wawache wazi nyuso zao na kutumia dalili za al-Albaani atakuwa amewavurumizia wanawake mlango ukawa wazi kwa kujishauwa uzuri wao hadharani na kuwahamasisha kufanya vitendo vya kulaumika vyenye kufanywa na wanawake wenye kuacha nyuso zao wazi siku hizi." Na katika ukurasa wa 233 akasema, "…na kuzikufuru Aya za Allaah." Hayo ndiyo yaliyokuwa maneno yake - twamuomba Allaah Amsawazishe na Amuongoze. Atasemaje kumuhusu Ibn al-Muflih, an-Nawawee, al-Qaadhi 'Iyyaadh na wanavyuoni wengine wa ki-Palestina, pamoja na Jamhuri ya wanavyuoni waliowatangulia wao na ambao ni ma-Salaf wangu kuhusiana na rai yangu katika mas'ala haya?"

5. Maafikiano ya at-Tuwaijree pamoja na waliopinduka mipaka katika kuzieleza vinginevyo ahaadeeth zilizo swaheeh zenye kukhalifiana na rai zao.

At-Tuwaijree alifanya hivyo katika hadeeth Khath'amiyyah. Walianzisha idadi ya mipangilio ya kimzaha katika kubatilisha kutumika kwake. Mimi nimewakosoa wote hao kwenye ar-Radd na mmoja wao katika Jilbaab al-Mar'ah al-Muslimah. Baadhi ya wanavyuoni wenye kuheshimika wamesema yakwamba hadeeth hiyo haina matamshi yaliyo bayana (yenye kubainika waziwazi) yakwamba uso wake ulikuwa uko wazi. Hizi ni miongoni mwa Rai zilizo mbali kabisa kutoka kwenye ukweli. Kwani, lau kama uso wake haungekuwa wazi, basi huyo mpokezi au mwenye kuona alipata wapi fikra hiyo yakwamba alikuwa ni mwenye kupendeza? Na al-Fadl alikuwa akitizamatizama kitu gani? Ukweli ni kwamba suala hili ni miongoni mwa dalili yenye nguvu zaidi yakwamba uso wa mwanamke si miongoni mwa 'awrah. Licha ya hayo, bado limebaki kundi lenye kusisitiza yakwamba alikuwa kwenye (au amevaa) Ihraam, haliyakuwa anajua yakwamba Ihraam yake haikumzuiya yeye na kujifunika na baadhi ya nguo zake juu ya uso wake. Wakati mwengine, at-Tuwaijree hukubali yakwamba uso wake ulikuwa wazi, lakini alikuwa akificha kuhusisha kwake kwa kusema, "Hapana ushahidi katika hilo yakwamba aliendelea kuuwacha uso wake wazi!" Alimaanisha yakwamba hwenda upepo labda wakati fulani ukamdhihirisha uso wake na lilipotokea hilo al-Fadl ibn 'Abbaas akamuona uso wake. Jee, yawezekana kwa muarabu kusema hivyo baada ya kuisoma hadeeth "al-Fadl akaanza kumuangalia na huku anamuelekea yeye," na katika riwaya nyengine "… kwahivyo akaanza kumuangalia na uzuri wake ukamshangaza." Hiki si kiburi na pembe mbili zilizochomoza? Wakati mwengine at-Tuweijree alikuwa akifasiri hilo kwa maana ya al-Fadhl alikuwa akimwangalia kipimo chake na umbile.

6. Kila mara kutumia ahaadeeth zisizo swaheeh na riwaya zisizotegemewa.

Kwa mfano, hadeeth ya Ibn 'Abbaas kuhusu kuliwacha wazi jicho moja peke yake imekuwa maarufu na kutumiwa na wale wenye kusisitiza yakwamba wanawake wanawajibika kufunika nyuso zao licha ya kujua kwao kuhusu udhaifu wake (hadeeth hiyo). Kwa hakika mmoja miongoni mwao pia aliithibitisha kuwa si swaheeh. Labda hadeeth iliyo muhimu zaidi katika hadeeth mashuhuri zisizotegemewa kuwa ni dalili ni ile iliyopokewa yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliyosema: "Kwani nyinyi nyote (wawili) ni vipofu?" Wamemfuata at-Tuwaijree na wengineo ki-Upofu katika madai yao yakwamba riwaya hii dhaifu imetiliwa nguvu na riwaya nyengine zenye kusaidia na kwamba ilikuwa ni dalili katika kukataza wanawake kuwaangalia wanaume, hata kama ni vipofu. Wamechukuwa msimamo huu licha ya ukweli yakwamba riwaya hiyo iliorodheshwa miongoni mwa riwaya dhaifu na wanavyuoni wakubwa katika ta'aluma ya uchambuzi miongoni mwao wakiwemo, kina Imam Ahmad, al-Bayhaqi na Ibn 'Abdil-Barr. Al-Qurtubee amesimulia yakwamba riwaya hiyo haikuzingatiwa kuwa ni swaheeh miongoni mwa wanavyuoni wa hadeeth. Kwahiyo, wanavyuoni wengi wa ki-Palestina walio katika madh-hab ya Hanbalee wamehukumu kwa msingi huo. Zaidi ya hayo, hivyo ndivyo inavyowajibika kwenye ilimu hii ya hadeeth na mifumo yake, kama ilivyodhihirishwa wazi kwenye al-Irwaa'.Hatahivyo, licha ya ushahidi wote huo kwa wenye kwenda

kinyume, Shaykh ‘Abdul-Qaadir as-Sindee akathubutu kuwa na Shaykh at-Tuwaijree pamoja na wengineo na wakadai yakwamba silsila ya upokezi wake ulikuwa ni swaheeh. Kwa kufanya hivyo, amejidhihirisha na ujinga wake au ujinga wa kujisingizia. Inasikitisha kwake kwa kuchukuwa msimamo huu, kwa sababu silsila (msururu wa wapokezi) ya hadeeth hiyo ina mpokezi asiyejulikana na ambaye kutoka kwake amepokea mtu mmoja tu pamoja na kuhitilafiana kwake na waliyopokea wanavyuoni wakubwa. Kinyume cha daraja ya uwanachuoni tuloizoea kutoka kwa Sheikh as-Sindee, ametanguliza katika kuunga madai yake mambo ya maajabu mno. Hoja zake, pasi na kutarajia zilikuwa na udanganyifu, upotofu, kufuata ki-Upofu, ufichaji wa ilimu, na kugeuka kutoka kwenye njia yake yeye mwenyewe ya kimsingi. Miongoni mwa misimamo ya kustaajabisha ni kwamba ujinga wa kujisingizia wa Sheikh as-Sindee yakwamba riwaya inahitilafiana na hadeeth ya Faatimah Bint Qays yenye ruhusa ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwake yeye (Faatimah Bint Qays) kuishi kwenye nyumba ya Swahaba kipofu, Ibn Umm al-Maktoom, ambaye atakaekuwa anaweza kumuona. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akatoa sababu kwa amri hiyo kwenye maneno yake kwake, “Kwani iwapo utavua kitambara chako cha kichwa, yeye hatokuona.” Katika riwaya ya at-Tabaree kutoka kwa Faatimah, alisema, “Aliniamrisha mimi niwe kwenye nyumba ya Ibn Umm Maktoom kwa sababu hatoweza kuniona mimi kila nitakapotaka kuvua kitambara changu cha kichwa.” Vilevile kuna idadi ya ahaadeeth nyengine zisizotegemeka zilizokusanywa na at-Tuwaijree katika kitabu chake. Mimi nimezitaja kumi kati ya hizo katika majibu yangu, na miongoni mwazo ni baadhi ya riwaya za uzushi.

7. Uainishaji wa baadhi ya ahaadeeth zilizo swaheeh na riwaya zilizothubutu kutoka kwa Maswahaba yakwamba si Swaheeh.

Wenye kupinduka mipaka wamezitangaza riwaya zilizothibitishwa na kutegemewa kuwa si za kutegemewa na ujinga wa kujisingizia wa kuzipa nguvu riwaya. Wakazidi kuzitangaza baadhi ya riwaya kuwa ni dhaifu mno, kama vile hadeeth ya ’Aaisha kuhusu mwanamke aliyefika umri wa kubaleghe, “Hafai kuonekana kiwiliwili chake isipokuwa uso wake na mikono yake.” Wameng’ang’ania kuitangaza kuwa si swaheeh - wajinga miongoni mwao wenye kuwafuata wengine ki-Upofu wasiokuwa na ilimu. Katika kufanya hayo, wamewakhalifu wale walio miongoni mwa wanavyuoni wa hadeeth walioipa nguvu kama vile al-Bayhaqi na adh-Dhahabee. Wengi wao, wakiwemo baadhi ya wanavyuoni mashuhuri, ujinga wa kujisingizia wa silsila zake za riwaya mbalimbali. Kwa hakika, at-Tuwaijree amesema waziwazi katika ukurasa wa 236 wa kitabu chake yakwamba maneno haya yamenukuliwa kutoka kwenye hadeeth ya ’Aaisha peke yake. Hata hivyo, amejionea kwa macho yake yeye mwenyewe katika ukurasa wa 57-9 katika kitabu changu silsila nyengine mbili: mojawapo ikiwa yatoka kwa Asmaa’ Bint ’Umays na nyengine kutoka kwa Qataadah kwa njia ya ufupisho (mursal) kwa silsila ya riwaya iliyo swaheeh. Wengi miongoni mwa wenye kufuata ki-Upofu wakamfuata, wakiwemo baadhi ya waandishi wanawake kama ilivyo kwenye Hijaabuki ukhtee al-Muslimah [Vazi lako, dadangu Muislamu], Ukurasa wa 33. Vilevile wakajifanya kuwa hawawajui viongozi wakubwa wa hadeeth na wengineo walioipa nguvu, kama vile al-Mundhiree, az-Zayla‘ee, al-‘Asqlaanee na ash-Shawkaanee. Baadhi ya wale wenye kujikuuza nafsi zao kuwa ni miongoni mwa wasomi wakubwa kwenye utaalamu huu wenye kuheshimika mno - akiwa kiongozi wao Sheikh as-Sindee - amedai yakwamba baadhi ya riwaya zake ni dhaifu sana na zisizotegemeka ili zipate kuepuka kutoka kwenye hukmu ya utaalamu wa hadeeth yakwamba riwaya zisizotegemeka hutiwa nguvu na riwaya zenye kufanana nazo.’ Katika kufanya hivyo, huwadanganya wasomaji wao wakadhani yakwamba hapana aliyewahukumu wapokezi madhaifu, kama ‘Abdullaah ibn Lahee‘ah, muaminifu na kwamba hawawezi kutumiwa kama ushahidi-msaidizi. Kwa kufanya hivyo, watakuwa wameukhalifu mfumo wa wanavyuoni wa hadeeth katika kutumia ushahidi-msaidizi. Miongoni mwao ni Imam Ahmad na Ibn Taymiyyah (رحمهم الله). Vilevile, wote wakajisingizia ujinga yakwamba wanavyuoni - miongoni mwao akiwemo Imaam ash-Shaafi’ee - ameithibitisha hadeeth kuwa ni mursal iwapo wanavyuoni wengi wataitumia kuwa ni ushahidi, kama ilivyo kwenye hadeeth ya ’Aaisha. Vipengele vyengine vyenye kutilia nguvu vinaweza kuongezwa kwenye hayo yaliyotangulia.

(a) Hadeeth hii imepokewa na Qataadah kutoka kwa ‘Aa’ishah.

(b) Imepokewa kwa silsila nyengine kutoka kwa Asmaa.

(c)Wapokezi wote watatu wa hadeeth hii wamehukumu kulingana nayo. Qataadah amesema katika tafsiri yake ya Aya ya kujifunika, “Allaah Amewafaradhisha wajifunike nyusi zao,” Yaani, “na wala sio kwenye nyuso zao.” kama ilivyosemwa na at-Tabaree. ’Aaisha amesema kumuhusu mwanamke akiwa kwenye Ihraam, “Anaruhusiwa kujifunika uso wake kwa kitambara, iwapo atapendelea kufanya hivyo.” Haya yamepokewa na al-Baihaqee kwa isnaad swaheeh ya wapokezi. Kuna ushahidi wa kutosha katika chaguo alilolitoa ’Aaisha kwa mwanamke mwenye kuhiji katika kujifunika yakwamba kulingana na rai yake, uso haukuwa ni ’awrah. Lau kama si hivyo, angelifanya jambo hilo kuwa ni waajib juu yao kama wale wenye kuyakhalifu hayo wanavyofanya. Kwa sababu ya msimamo wao, wengi wa waandishi wenye kupinduka mipaka, wakiongozwa na at-Tuwaijree, wameyaficha haya matamshi ya Ummul Mu’mineen, ’Aaisha mbali na wasomaji wao. Mtunzi wa Faslul-khitwaab, amefuta kifungu hiki cha al-Baihaqee kwa makusudi kutoka katika kitabu chake. Na hili likiwa ni mojawapo tu ya idadi ya vitendo vya utovu wa heshima nilivyovibainisha kwenye kitabu change. Ushahidi-msaidizi ni kwamba riwaya hii iliyo swaheeh kutoka kwake unaitilia nguvu hadeeth yake kutoka kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم). Haya ni miongoni mwa ukweli ambao wengi hawaujui au wanajifanya kuwa hawajui, emma chaguo limekuwa ni uchungu kulimumunya. Ama kumuhusu Asmaa’, imeswihi kupokewa kutoka kwa Qays ibn Abee Haazim yakwamba alimuona yeye kama mwanamke mweupe aliye ta michoro (tatoos) kwenye mikono yake.

(d) Riwaya ya Ibn ‘Abbaas iliyotajwa hapo awali, “Na aivute Jilbaab (kitambara) karibu na uso wake bila ya kuiweka kwenye uso wake.” Tafsiri yake ya Aya ya mapambo “... Isipokuwa yale yenye kudhihirika” kuwa yanahusu “uso na mikono” ilikuwa ni kama hiyo. Vilevile kuna riwaya inayofanana na hiyo kutoka kwa Ibn ’Umar yenye mashiko hayohayo. Katika nukta hii, ukweli wenye uchungu ni lazima utambulike kutokana na mafunzo yatakayopatikana ndani yake, ilimu yake na kutumika kama msemo wa ukumbusho: “Ukweli haujulikani kwa watu, ujuwe ukweli na

utawajua watu wake." Wakati uleule ambao Sheikh at-Tuwaijree anaposisitiza kuikataa hadeeth ya 'Aaisha na ushahidi wenye kusaidia, miongoni mwao ikiwemo riwaya mursal ya Qataadah, amelazimika kuikubali hadeeth nyengine isiyo swaheeh kutoka kwake ('Aaisha) ikiwa na usaidizi-mursal. Katika hadeeth hiyo imetajwa "... Yakwamba alivaa Niqaab (kitambara chenye kufunika uso wake) ..." na kwamba alikuwa amehitajika kumueleza alivyokuwa mkewe Mtume (صلى الله عليه وسلم), Swafiyyah, na wanawake wa ki-Answaar kuwa "... Ni mwanamke wa ki-Yahudi miongoni mwa Mayahudi wanawake ..." jambo ambalo lililozingatiwa na wanavyuoni kuwa ni matamshi yenye makosa makubwa sana (munkar Jiddan). Sheikh ameleta hoja katika ukurasa wa 181, "Inayo ushahidi wa usaidizi wa mursal," na akanukuu mojawapo ya hadeeth mursal ya 'Ataa' iliyo na mrongo ajulikanae kwenye silsila yake ya upokezi. Mtu na atafakari juu ya tafauti kubwa baina ya ushahidi huu wa kuzua wenye usaidizi na ushahidi ulio swaheeh na wenye usaidizi wa Qataadah uliopata usaidizi zaidi kutokamana na ushahidi mwengine, kisha uulize, "Ni kwanini at-Tuwaijree akaikubali hadeeth ya pili ya 'Aaisha na wala asiikubali ya kwanza?" Jawabu ya wazi ni kwamba iliyokubaliwa imetaja mas'ala ya kuvaa niqaab - hata kama haikuashiriya uwajibikaji - haliyakuwa iliyokataliwa imeyakataa hayo. Kwahiyo, katika hali hii, Sheikh hakuegemeza msimamo wake juu ya Msingi wa kisheriya wa Ki-Islamu, lakini juu ya kitu chenye kufanana na Msingi wa ki-Yahudi usemao: "Mwisho wa jambo huhalalisha Njia". Twamuomba Allaah Atuhifadhi sote.

8. Kuweka masharuti yasiyokuwa ya Busara.

Miongoni mwa mambo yenye kushangaza kwa baadhi ya wanavyuoni wa kisasa wenye kufuata ki-Upofu katika madh-hab ya ki-Hanafi na wengineo ni kwamba kwa upande mmoja hukubaliana na sisi kuhusiana na kuruhusiwa kwa wanawake kuacha wazi nyuso zao, kwa sababu hiyo ndiyo iliyokuwa misimamo ya ma-Imaam wao, lakini kwa upande mwengine wanakubaliana na wenye kupinduka mipaka katika kuwakhalifu ma-Imaam wao. Wao hufanya Ijtihaad (wakidai kufanya taqleed) kwa kuongeza sharuti yakwamba mujtama' usalimike na fitna ya misimamo ya ma-Imaam. Hii inahusiana na fitna inayosababishwa na wanawake kwa wanaume. Kisha mjinga mmojawapo anaefuata ki-Upofu wa siku hizi akazidi kwenda ukingoni kwa kunasibisha haswa "sharuti hili" kwa ma-Imaam wenyewe. Miongoni mwa baadhi ya wale wasiokuwa na ilimu, hili likawasababisha wao wakatikiwe yakwamba kimsingi hapana tafauti baina ya misimamo ya ma-Imaam na wenye kupinduka mipaka. Ni wazi kwa wanavyuoni yakwamba sharuti hili halifai kwa sababu linaleta maana yakwamba wana-adamu hujua mambo ambayo Mola ameshindwa kuyatambua. Yaani, ushawishi wa wanawake katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) haukuwepo, kwahiyo inatubidi kuleta hukmu maalum ambayo haikuwepo hapo awali. Kwa hakika, fitna hiyo ilikuwepo katika zama za kuteremshwa kwa ujumbe wa kisheriya na kisa cha al-Fadhl Ibn 'Abbaas cha fitina na mwanamke wa Khath'amiyyah na kumtazama kwake mara kwa mara ni jambo lisilo mbali na fahamu za wasomaji. Ni jambo lenye kujulikana yakwamba Allaah (سبحانه وتعالى) aliwaamrisha wanaume na wanawake waangushe macho yao na akawaamrisha wanawake wajisitiri kisawasawa mbele ya wanaume. Alifanya hivyo ili azibe njia zenye kuelekea kwenye ufisadi na kuzuia ushawishi. Licha ya yote hayo, Allaah (سبحانه وتعالى) hakuwaamrisha wanawake wafunike nyuso zao na mikono yao wakiwa mbele yao. Mtume (صلى الله عليه وسلم) haukuwepo, akazidi kutilia mkazo katika kisa cha al-Fadhl kwa kutomuamrisha mwanamke aufunike uso wake. Na Allaah Alikuwa ni Mkweli pindi aliposema, "Na Mola wako si mwenye kusahau." Ukweli ni kwamba sharuti la kutokuwepo fitna lilitajwa na wanavyuoni tu kuhusu mwanamume anapomtazama mwanamke uso wake, ama katika "al-Fiqh 'alaa al-mathaahib al-arba'ah, uk. 12, wamesema yakwamba, "[Uso wa mwanamke unaweza kuwachwa wazi] Inaruhusiwa kwa sharuti yakwamba kutapatikana usalama kutokana na ushawishi," na hayo ni kweli, kinyume cha wanavyofanya wenye kufuata ki-Upofu. Wamekatikiwa kutokana na hayo yakwamba mwanamke anawajibika kufunika uso wake, haliyakuwa kwa hakika si kipengele muhimu. Wanajua yakwamba sharuti la usalama kutokamana na ushawishi vilevile unawahusu wanawake. Kwani hairuhusiwi kwao kutazama nyuso za wanaume isipokuwa iwapo kutakuwa na usalama kutokamana na ushawishi. Jee, kwani ni kipengele muhimu kwa wanaume nao kujifunika nyuso zao wasionekane na wanawake kulinda ushawishi kama baadhi ya makabila wanaoitwa Tawareg wafanyavyo? Wangelikuwa na msingi kwenye fiqh ya Qur'an na Sunnah iwapo watasema yakwamba mwanamke aliyevaa jilbaab kisawasawa, akawa anahofia kudhuriwa na baadhi ya watu mafatani kutokamana na kuuwacha wazi uso wake awajibike kuufunika uso wake kulinda madhara na ushawishi. Kwa hakika, hwenda pia ikasemekana yakwamba ni wajibu juu yake asitoke nyumbani kwake iwapo atahofia yakwamba baadhi ya wenye mamlaka waovu wenye kusaidiwa na kiongozi asiyehukumu kwa aliyoyateremsha Allaah, kama ipatikanavyo kwenye baadhi ya nchi za kiarabu tangu miaka michache iliyopita, walikuwa wakimvua jilbaab kutoka kwenye kichwa chake. Ama kufanya uwajibikaji huu kuwa ni wa lazima kwa wanawake wote kila mahali na kwenye zama zote, hata kama hapakuwepo na madhara yoyote kwa wanawake waliojisitiri, Laa, Hilo haliwezekani kabisa. Allaah daima ni mkweli pindi aliposema, "Wao wana washirika wenye kuwawekea wao amri (za kisheriya) kwenye dini ambazo Allaah asizowaekea?" Haya ndiyo makosa ya wenye kupinduka mipaka yaliyodhihiri ambayo niliyoyafikiriya kuyapa utajo kwa mukhtasar kutokana na mafungamano yake na yaliyomo kwenye kitabu hiki. Kisha namalizia kitabu hiki "ar-Radd al-Mufhim" kwa kuwakumbusha yakwamba kupinduka (kuvuka) mipaka katika dini - tukizingatia yakwamba Allaah ameyakataza na wala hayaleti mazuri yoyote. Na hayawezi kuleta kizazi cha mabinti wa ki-Islamu watakaobeba ilimu ya Uislamu na kufanya matendo juu ya mfumo wa kati na kati, pasi na ziyada wala upungufu. Sio kama niliyowahi kuyasikiya kuhusu baadhi ya mabinti wa ki-Islamu kwenye nchi za kiarabu pindi waliposikiya maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم), "mwanamke mwenye Ihraam hafai kuvaa niqaab wala Glavu!" Hapana shaka, haya ndiyo matokeo ya rai za wenye kuvuka mipaka waliyoyasikiya kuhusiana na uwajibu wa kufunika nyuso zao. Kwa hakika mimi siamini yakwamba sampuli hii ya kuvuka mipaka - na huu ni mfano mmoja tu kutokamana na mengi niliyo nayo yenye uwezo wa kutuletea wanawake wa ki-Salafee watakaokuwa na uwezo wa kufanya kila jambo lenye kuwajibishwa na uongofu wa kidini katika maisha ya kijamii kulingana na walivyokuwa wanawake wema wa ma-Salaf.